



**PROGRAM**

**1**

*UNANGOJA NINI? JIANDIKISHE KUSHIRIKI SASA*

IJUE TASNIA YA UTALII NA AJIRA ZAKE /CAREER DEVELOPMENT IN TOURISM

*Utangulizi*

Maruku Paradise Beach ikishirikiana na Kiroyera tours Bukoba na Mama Mary Kalikawe (mama huyu nimboenzi katika ualimu na ni mama muandamizi katika tasnia ya Utalii), wamejipanga kutoa mafunzo ya bila malipo, ya somo tajwa hapo juu ambalo ni Ijue Tasnia ya utalii na ajira zake. Mafunzo haya yanawalenga wananchi kwa ujumla na hasa waendeshaji wa tafrija na matukio, vijana wanaotegemea kuingia kwenye ajira mbali mbali, waalimu, wanahabari, na pia watu wanaohusika na mipango ya maendeleo ya nchi yetu.

Mafunzo haya yatatolewa siku za Jumamosi mbali mbali huko Maruku Paradise Beach (Usafiri kutoka Bukoba mjini na kurudi utaandaliwa kwa wale watakojiandikisha kushiriki katika mafunzo haya ya sikumoja). Cheti cha ushiriki kitatolewa.

Washiriki wa mafunzo watatakiwa kufika MPB saa tatu asubuhi na mafunzo yataendelea kutoka saa tatuhadi saa nane mchana. Mafunzo yatatolewa kwa nadharia na kwa vitendo

*Kwa nini wazo la kutoa mafunzo haya?*

Utalii ni nguzo ya uchumi. Watu wengi hawaingii katika kutengeneza ajira za tasnia ya utalii kwa sababuhawaijui vizuri tasnia hii. Katika watu mia tuliowauliza aina za kazi katika utalii, ni asilimia 20 tu ambao walionesha uelewa wa ajira katika mnyororo wa thamani ya Utalii.

Wazazi wanasita kupeleka watoto wao katika shule za utalii kwa kuchelea vijana wao hawatapata ajira. Hii ni kwa sababu hakuna uelewa wa jinsi ya kujajiri wenyewe

Mhe Rais amefufua vitu vingi ambavyo vinasemekana ni kwa ajili ya kukuza utalii ikiwemo shirika la ndege ATC, Treni ya Umeme, Meli za maziwa mbali mbali, bidii kwa mabalozi wa Tanzania nchi mbalimbali wanatakiwa kutangaza uwekezaji na pia utalii Tanzania. Wizara ya mali asili na utalii nayo inaonekana kuwika, lakini uelewa wa watu juu ya utalii na jinsi unavyojenga uchumi hasa kwa kutengeneza ajira bado ni mdogo.

*Malengo na matokeo ya kuhudhuria mafunzo haya:*

1. Washiriki watakuwa wameongeza upeo wao wa uelewa, na hii itawaongezea upendo namsukumo wa kuchukua ajira katika tasnia ya utalii.
2. Kwa wale ambao tayari wako kwenye ajira ndani ya tasnia hii, mafunzo haya yataoneshamaeneo ya utendaji yenye udhaifu na namna ya kuongeza uzalishaji.

3. Wanamipango ya maendeleo watajua maeneo katika mipango ya muda mrefu ambamo ajira zautalii zinachangia katika mipango hiyo.

*Yaliyomo katika mafunzo haya:*

1. Ujue utalii na aina za utalii
2. Mnyororo wa thamani wa utalii
3. Ajira katika mafundo ya mnyororo wa thamani
4. Kujijiri katika Utalii
5. Maeneo ya udhaifu katika utendaji na uzalishaji katika utalii
6. Ajira za utalii na mipango ya maendeleo ya uchumi wa

mkoa/nchiMWISHO

### **Mafunzo ya kwanza ni Jumamosi tarehe 13 March 2021**

Usafiri kutoka Bukoba mjini utaondoka saa moja na nusu Asubuhi Banan Hotel kuelekea MPB na kurudimjini saa tisa mchana

Gharama za usafiri wa Hiece kutoka Bukoba mjini na kurudi sh 5,000/=

Gharama ya Chakula, chai na kinywaji kimoja Sh 10,000/=

Jumla Sh 15,000/=

Kama utapenda nyama choma na vyakula vingine utanunua kwa gharama yako. Unaweza pia kununua vinywaji unavyotaka wewe kwa gharama yako



Mama Mary Kalikawe ni mwalimu wa muda mrefu. Amefundisha Chuo kikuu cha Dar es salaam, Chuo kikuu huria Tanzania na kuwa Mkuu wa chuo cha utalii na wanyamapori nchini Botswana. Amekuwa mkurugenzi katika bodi ya utalii Tanzania na ni mwanzilishi wa Utalii mkoani Kagera akiwa mkurugenzi mwendeshaji wa Kiroyera Tours. Ni mwenyekiti wa chama cha wanawake walio katika fani ya utalii Tanzania (AWOTTA) na Mama Mary ni Balozzi katika Bodi ya Utalii Africa.



Kiroyera Tours ni kampuni ya utalii kongwe hapa Tanzania ambayo ilianzisha utalii mkoani Kagera miaka 20 iliyopita. Imepokea watalii wengi wa ndani na nje ya nchi, imetoa mafunzo kwa vijana mashuleni na kuendesha semina mbali mbali. Kiroyera ina matawi mawili mjini Bukoba na Dar es salaam



Maruku Paradise Beach ni eneo zuri kwenye ufukwe wa Ziwa Victoria, liko kilometa 26 kusini mwamji wa Bukoba. Kuna eneo la kupata mafunzo, vyakula, vinywaji na burudani kama kuogelea na kufurahia beach na upepo mwanana wa ziwa.

Kwa Mawasiliano na kujiandikisha kushiriki:

Simu: 0759424933 ipo pia whatsapp

Email: [mkalikawe@gmail.com](mailto:mkalikawe@gmail.com)